**Jina ……** **Nambari Yako ……**

**Shule ……** **Sahihi ……..**

**Tarehe …….**

**102/2**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**(LUGHA)**
**JULAI / AGOSTI 2009**
**MUDA: SAA 2½**

# MITIHANI YA MAKADIRIO YA PAMOJA
# WILAYA YA MASABA (KIRIMA) - 2009
***Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)***

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
MUDA: SAA 2 ½

**MAAGIZO:**

- Jibu maswali
- Maswali yako yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika karatasi hii ya maswali

**KWA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1. Ufahamu | 15 | |
| 2. Muhtasari | 15 | |
| 3. Matumizi ya lugha | 40 | |
| 4. Isimu Jamii | 10 | |
| Jumla | 80 | |

*Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa, watahiniwa lazima wahakikishe kurasa zote zimepigwa chapa sawa sawa na kuwa maswali yote yamo.*

**1. UFAHAMU**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Limeibuka swala kwamba polisi waliokuwa wakiongoza mashtaka mahakamani sasa watakuwa chini ya himaya ya Mkuu wa sheria si kamishina wa polisi. Ni hatua iliyo na mashiko katika utekelezaji na usimamizi wa sheria.

Hatua hiyo itasaidia kuhakikisha kwamba washtakiwa watapata haki kamili na kuzuia visa ambapo polisi wakati mwingine walikuwa wakiwasingizia washtakiwa madai ya uongo na kasha kuwatolea mashtaka.

Polisi hawapaswi kutekeleza majukumu Fulani katika maongozi ya sheria kwa kuruhusiwa kuwatia nguvuni washtakiwa, kuwatayarishia mashtaka na halafu kuwafikisha mahakamani.

Maafisa husika sharti wafunzwe upya kuongoza mashtaka kuambatana na sheria wala si kanuni za polisi wanaoongoza mashtaka, wawe mawakili waliosomea uanasheria ipasavyo sawa na mawakili hao wengine. Hali hii itazuia visa ambapo wakili huwa anafahamu sheria kuliko kiongozi wa mashtaka.

Mawakili zaidi wa umma wafaa kutengewa wasio na pesa za kuwalipa mawakili wa kibinafsi kuwatetea. Hatua hizo zitaharakisha kesi zirundikanazo mahakamani na kupunguza idadi ya washtakiwa wanaowekwa rumande kutokana na hitilafu za kisheria.

**MASWALI**

a) Yape makala haya anwani mwafaka (alama 1)

……

……

b) Kwa mujibu wa makala fafanua jinsi utekelezaji wa sheria mahakamani umetiwa sura mpya (alama2)

……

……

……

……

c) Thibitisha kuwa washtakiwa nchini Kenya wamekuwa wakikosa haki. (alama2)

……

……

d) Shughuli za mahakama na utekelezaji sheria zahitaji kuboreshwa. (alama3)
Eleza

……

……

……

…….

e) i) Orodhesha majukumu ambayo polisi hawafai kuyatekeleza kisheria (alama 2)

…….

…….

ii) Eleza kwa nini unadhani polisi nchini hawajawajibika (alama1)

…….

…….

iii) Eleza sababu muhimu inayowakataza polisi kutekeleza majukumu uliyoyaorodhesha katika sehemu ya (e) i) (alama1)

…….

…….

f) Eleza maana ya (alama3)

i) Rumande …….

ii Himaya ……

iii) Zirundikanazo …….

## 2 MUHTASARI / UFUPISHO

**Soma taarifa ifuatayo kisha uyajibu maswali**

Nchi nyingi duniani zimetia saini mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watoto. Haki ni mambo mema ambayo watoto wanastahili kutendewa. Kwa kutia saini, nchi hizi zimetangaza kujitolea kwao kuzilinda na kuhakikisha kuwa hakuna ukiukaji wake na kuwa watoto wote katika himaya zao wananufaika kutokana na haki hizi.

Miongoni mwa haki hizi ni kuwa kila mtoto ana haki ya kuishi na kupata chakula cha kutosha na chenye vimilishe bora. Pili, kila mtoto ana haki ya elimu. Elimu hii inafaa kutolewa bila ada na iwe inayofaa na inayopatikana kwa urahisi. Kisha, kila mtoto ana haki ya kutopigwa, kutodunishwa, kufanya kazi za kitumwa, nzito na za kushurutishwa. Halikadhalika ana haki kuishi katika nyumba au makazi bora na salama, kutunzwa na kulindwa dhidi ya hali yoyote inayoweza kumhatarisha. Anatakiwa ashirikishwe katika kufanya maamuzi. Fauku ya haya, ana haki ya kupata huduma za afya, mahitaji maalumu, michezo, upendo na habari. Isitoshe anastahili kuheshimiwa kimawazo na kihisia. Haki hizi zinatakiwa kulindwa na kila mwanajamii, hivyo serikali za mataifa mengi zimeshirikisha haki hizi katika katiba za nchi zao na sheria zao.

Walakini, haki hizi bado zinakiukwa. Watoto wengi kote duniani bado wananyimwa haki zao. Lakusikitisha na kukera ni kuwa wanaotarajiwa kuwa vigogo vya kuzilinda haki hizi ndio wanaongoza kuzikiuka. Kila siku tunasikia na kushuhudia visa vya watoto kupigwa, kunyimwa chakula, kufanyishwa kazi kipunda, kuteswa, kuishi katika mazingira hatari na hata kuuawa. Kuna watoto wengi wanaolala nje. Wengine hawapati chakula, licha ya kuwa wanatakiwa kupata

chakula chenye lishe bora. Kwao kutarajia mlo awamu tatu kwa siku ni njozi kwani hata awamu moja ni adimu kupata.

Watoto wengi katika mataifa yenye fujo na ghasia hutekwa na kutumikishwa vitani. Viongozi katika mataifa haya hawafanyi kitu ila kutazama tu wakati watoto wanaotakiwa kuwalinda wamegeuka mibaba ya kuua na kuuana. Watoto hawa huvishwa magwanda ambayo miili yao minyonge haiwezi kuyahimili. Pia huvalishwa mabuti ya kijeshi ambayo ni mizigo mizito ya kubeba mbali na bunduki zinazokaribia kuwazidi uzani wakati wanatakiwa kuwa wamelindwa majumbani na shuleni na wazazi wao na serikali.

Jukwaa la vijiji vya mataifa ya ulimwengu wa tatu limesheheni watoto wasioenda shule kwa sababu ya lindi la ufukara uliokithiri. Elimu ya bure inayogusiwa katika haki za watoto haipo. Wanaong'ang'ana iwepo ni kama kwamba ni waota ndoto mchana. Jiulize, watoto wangapi sasa hivi wamo majumbani bila kwenda shuleni kutokana na ukosefu wa karo? Wangapi wamo mitaani wakivuta na kunusa gundi huku wakiombaomba vishilingi?

Hivi ilivyo sasa hivi inadai kuwa mimi na wewe tufanye hima na kuungana mikono kutafuta suluhisho la kudumu kuhusu haki za watoto. Twapasa kuhimiza serikali zetu kufanya kila ziwezavyo kuhakikisha kuwa watoto wote wako shuleni. Nasi tushirikiane kutoa huduma kwa watoto na kukomesha dhuluma, mateso na dhiki kwao. Haitoshi kupeleka miswada bungeni kuhusu haki za watoto na kuipitisha kuwa sheria. Twastahili kubadilisha misimamo yetu kuhusu haki hizi na kuzilinda kwa dhati bali si kwa chati.

**2. MASWALI**

a) Fupisha aya mbili za kwanza (maneno 65 – 70) (alama 8)

Matayarisho

…….
…….
…….
…….
…….
…….
…….
…….

Jibu

…….
…….
…….
…….
…….

…….

…….

…….

b) Eleza ni vipi ukiukaji wa haki za watoto unaweza kuepukwa (maneno 30 – 35) (alama4)

Matayarisho

…….

…….

…….

…….

…….

…….

…….

…….

Jibu

…….

…….

…….

…….

…….

…….

…….

…….

Kumbuka alama za mtiririko ni 3

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

a) Ainisha sentensi ifuatayo.

Mwanafunzi yule anaandika haraka sana (alama 2)

…….

…….

b) Nyambua vitenzi vifuatavyo vya silabi moja ili kujaza mapengo (alama 2)

i) Mgeni ali …….. (pa, kutendewa) kiti ili akae

ii) Ame …… (la, kutendesha) mtoto chakula

c) Toa <u>maana</u> mbili ya sentensi hii (alama 2)

Nionyeshe vile nitakavyobeba

i) …….

…….

ii) ……

……

d) Badilisha kwa msemo halisi (alama 3)

Raisi alisema kuwa angesafiri kwenda Dubai siku hiyo alasiri

……

……

……

e) Kwa kutolea mifano ya sentensi, bainisha matumizi matatu ya ritifaa (kibainishi) (alama3)

i) ……

……

ii) ……

……

iii ……

……

f) Tumia viunganishi hivi <u>mwanzoni</u> mwa sentensi kuonyesha matumizi yake (alama 2)

i) Ikiwa …..……

……

ii) Labda …….……

……

g) Geuza sentensi ifuatayo katika ukubwa (alama 2)

Mtoto alitishwa na mtu mrefu ajabu

……

……

h) Andika upya sentensi hii ukifuata maagizo (alama 2)

Kalamu ilipopotea, mwalimu alikasirika

(Anza: Kupotea …….)

……

……

i) Eleza matumizi ya –po katika sentensi zifuatazo (alama 2)

i) Nyerere <u>ajapo</u>, tafadhali mwambie anione

……

……

ii) Mtoto alia<u>po</u>, kijakazi humpa chakula

……

……

j) Tunga sentensi mbili kuonyesha viwakilishi vionyeshi katika ngeli ya li – ya (alama 2)

i) …….

…….

ii) …….

…….

k) Tunga sentensi kwa kutumia nomino zifuatazo na kuvumishi – ingine (alama 2)

i) Samaki…….

…….

ii) Kuchezacheza …….

…….

l) Kanusha sentensi zifuatazo kwa wingi (alama 2)

i) Yeye akiachwa pekee, ataivuruga kazi

…….

…….

ii) Nikichapishiwa riwaya hii, nitafurahi

…….

…….

m) Andika vitenzi vitatu na uonyeshe viwakilishi nafsi viambata kwa umoja (alama 3)

i) ……

ii) …….

iii) …….

n) Onyesha mzizi wa kila kitenzi katika orodha ifuatayo (alama 4)

i) Hawajala …….

ii) Walipiganishwa ……..

iii) Waliendesheana ……..

iv) Sikumkuta ……...

o) Bainisha vishazi vilivyotumika katika sentensi hii.

Aliyemchukua mjini amemwajiri kazi (alama 2)

…….

…….

p) Sauti hizi ni za aina gani? Na hutamkiwa wapi?

IjI …….

IghI …….

q) Onyesha upatanisho wa kisarufi na vivumishi visisitizi wa nomino ifuatayo (alama 1)

Malkia …….. alisumbuliwa sana na raia wake. (alama 3)

**SWALI LA 4**

**4. ISIMU JAMII**

Wakili: Wewe ndiwe Rose Kerubo mtoto wa Oyondi?

Kerubo: Ndio mheshimiwa.

Wakili: Waweza kueleza mahakama haya mnamo tarehe 22/05/09 ulikuwa wapi na akina nani mkifanya nini?

Kerubo: Bw. Mheshimiwa wakili, ama kwa hakika siku hiyo mimi na wenzangu tulikuwa safarini nchi utubora.

Wakili: Je wajua kwamba kesi hii kulingana na kifungu cha 213 sehemu ya ……..

a) Andika muktadha wa mazungumzo haya (alama 2)

…….

…….

…….

…….

b) Taja sababu za wakili kutumia marejeleo mengi katika mahojiano yake (alama 2)

…….

…….

…….

…….

c) Huku ukirejelea kikao chochote cha shughuli ya mahakama eleza sifa za lugha itumikayo huko. (alama 6)

…….

…….

…….

…….



**Mwisho**